# MIAKA ELFU YA UTUKUFU

*I Korintho 2:9-10, Lakini kama ilivyoandikwa mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho, maana Roho kuchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.*

*Isaya 27:13 Tena itakuwa katika siku hiyo, tarumbeta kubwa itapingwa, nao waliokuwa karibu na kuangamia katika nchi ya Ashuru watakuja na hao waliotupwa katika nchi ya Misri; nao watamsujudia Bwana katika mlima Mtakatifu huko Yerusalemu.*

Hebu sasa natuangalie nini Nabii wa Mungu amesema kuhusu somo hili muafaka. Ni wakati wa kutoka. Ni wakati mzuri wa kuitwa kutoka na kwenda kwenye nchi ya ahadi, sio ahadi ya kwenda nchi nyingine bali nyumbani, utawala wa miaka elfu, muda wa kutoka, uovu wa Taifa hili umejaa, limekuwa chafu.

Sasa nataka wewe ufahamu, nguzo ya moto iliyoongoza Israel kwenda nchi ya ahadi inaongoza watu tena kwenda nchi ya ahadi utawala wa miaka elfu, tunaiona katika ufunuo wa Muhuri wa sita (Rev, 6:12-17) ambao haujafundishwa kabla, jinsi dunia itakavyotakaswa ili kuingia kwenye utawala wa miaka elfu. Nguzo ya moto inawaongoza kweye utawala wa miaka elfu.

Fahamu nguzo ya moto iliyowatoa Israel katika utumwa katika Kutoka; nguzo ya moto, chini ya uongozi wa Mungu, Mungu ndiye ule moto na nguzo ya moto ndiyo tu inayompaka mafuta Nabii. Nguzo ya moto ilisimama kama shahidi wa Mbinguni kwamba Musa aliitwa atoke (kutoka 13:21-22, 14:19-24).

Lakini kwa muda huu (utukufu kwa Mungu) Nguzo ya moto tunayoiona miongoni mwetu, nguzo ya moto inatuongoza kwenye utawala wa miaka elfu ambapo atarudi kwa watu wake katika utawala ule Mkuu wa miaka elfu baada ya kutoka, tutakapoishi milele pamoja naye Yeye muda wote analo Neno la Baba, siku zote inathibitisha hiyo ni kweli.

Kutoka kwa kwanza, alifanya nini? Aliwatoa kutoka katika nchi ya asili kwenda nchi ya asili. (Kutoka Misri kwenda Kanani) kutoka kwa pili anatutoa kutoka hali ya kiroho kwenda kwenye ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu (Matendo 2:14 – 36) sasa anawaleta kutoka ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu kwenda kwenye nchi ya milele ya utawala mkuu ujao wa miaka elfu
(Ufu. 20.4-6, 5:9:-10).

Sasa tunaona kwamba karamu ya arusi ikaribu. Sasa kama hatutaonana tena, kumbuka karamu ya Arusi ikaribu . na pia ufalme kufuatana kama tulivyo-ahidiwa uko tayari kusimamishwa Milenium kuu, kuchukuliwa kwa Kanisa na kuharibiwa kwa waovu na Ulimwengu chini ya mhuri wa sita, utatakaswa na volkano kuondoa uozo wote na dhambi za ulimwengu (Isaya 13:6-13) na kuiumba upya na kuleta utawala wa miaka elfu mpya kwa wakati ujao. Wakati tunaangalia mafunuo haya matatu yaliyofungwa. Mungu katika Kristo, Kristo katika Kanisa, ufalme unaokuja. Adam na Hawa wamekombolewa tena na kurudishwa katika bustani ya Eden kuwawakilisha Kristo na Bibi Arusi. Na ufalme utakwenda kurudishwa kufuatana na ahadi yake. Utukufu kwa Mungu.

Wakati wakuja kwake Bwana Yesu, wale wanaopenda hasa kule kuja kwake na kwamba wanaishi kwa hilo atakapotokea Mawinguni, wale walio kufa katika Kristo watafufuliwa na wengine waliohai watabadilishwa mara moja. (1 The 4:13-17, Phil 3:20-21) wengine waliobaki hawatajua hilo. Kumbuka alitokea kwa wale waliokuwa mjini, Unaona unyakuo utakuwa kama hivyo, vema angalia tutaonana mmoja kwa mwingine vema tutawaona wao. Waliobaki ulimwenguni hawatawaona. Watanyakuliwa na kuondoka kisiri, tunangojea kwa wakati huo. Halafu tutarudi tena Duniani kwa utawala wa utukufu wa miaka elfu moja. Waliobaki mautini hawataishi miaka elfu, na baadaye utakuja ufufuo wa jumla ambapo Israel wote ……. Ufunuo 20:11-15.

Sasa tunaona pia katika muhuri wa sita sasa umefunguliwa, ulikuwa kwa makusudi matatu yaliyofungwa. Sasa haya yalikuwa madhumuni, kitu cha kwanza wale wanawali wapumbavu watakwenda kwenye kipindi cha mateso, dhiki kuu kwa kusafishwa (Ufu. 6:12-17) watatakaswa dhambi zao za hutoamini na kukataa ujumbe. Hilo litafanywa wakati wa kipindi cha mateso (dhiki kuu). Tunaona anaonekana kwenye ufunuo 7 kati ya mlango wa 6 na 7 hapa amekwisha takaswa, na amepewa vazi lake (Ufu. 7:13-17)

Sasa sio, Bibi Arusi, sasa ni Kanisa ni watu halisi ambao hawakupata nafasi, labda kupokea ujumbe, au kwa njia moja au nyingine walipofushwa na hawa manabii wa uongo, na hawakupata nafasi, bado ni waaminifu moyoni mwao, na Mungu anaifahamu mioyo yao na hapa walitakaswa katika kipindi hicho.

Uelewe kipindi kingine cha kutakaswa. Ni wakati Israel wanapokusanyika pamoja. Hilo ni kusudi la pili. Mungu atawatakasa Israel katika kipindi cha mateso Daniel 12:1-13, Jeremia 30:4-9. Nje ya mamillion waliojikusanya pale, kuna waliochaguliwa mia moja arobaini na nne. Elfu, watatakaswa pia (Uf. 7:1-8, Zakaria 13:4-9) Mungu anatakasa Israel.

Angalia kuna Ulimwengu mzima nao inabidi utakaswe kutakuwa na vitu kama vile mwezi, nyota, na vitu vyote vya asili vitakaswe Unaona ni nini? Ulimwengu unajifanya upya wenyewe unatakaswa uwe tayari kwa utawala wa miaka elfu.

utawala wa miaka elfu unakuja. Kila kilicho kichafu inabidi kitakaswe kwenye muhuri wa sita (Isaya 24:1-6, Matt. 24:29-31).

Sasa, sasa, unafahamu katika kufunguliwa kwa muhuri wa saba ni siri iliyofungwa katika mafungu matatu. Hiyo moja ninayo. Itanena na imenena nayo ni siri ya zile ngurumo saba. Ngurumo saba za Mbinguni zinafungua siri, itakuwa wakati wa kuja kwake Kristo. Sababu Yesu alisema hakuna atakayefahamu siku atakayo rudi (Mat. 24:32-44, Ufu. 8:1-5 na Uf. 10). Wakati wa utawala wa miaka elfu unapoanza, jinsi gani wasioamini watakavyo ondolewa toka duniani? Wasioamini watakwenda kwenye kipindi cha mateso (dhiki kuu) pamoja na wanawali wapumbavu na wengine wote (wasioamini na wanawali wapumbavu) na mabaki ya Israel ambao watachukuliwa watoke.

Watakuwa wapi wanawali wapumbavu kwenye utawala wa miaka elfu? Katika utawala wa miaka elfu watakuwa makaburini. Wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie miaka elfu." Ufunuo 20:5.

Utawala wa miaka elfu utakuwa miaka elfu au ni namba tu? Ni miaka elfu (Ufunuo 20:4:6) siogopi ulimwengu ukiwa vipande vipande. Utakuwepo utawala wa miaka elfu wakati huu utakapoisha. Mungu hawezi kulipinga kusudi lake, kitu kimoja niombe, "Bwana niko sahihi kwenda wakati ujapo? Hilo ndilo pekee ninalolihofia je nimekupendeza. Bwana?. Unaona Usiogope watu wanachofanya jali Mungu anachosema"Usiogope anayeuwa mwili ogopa yule anayeuwa mwili na roho katika kuzimu" (Mat. 10:28).

Kutakuwepo na ufufuo wa wafu atalihakikisha hilo, hiyo ni kweli atalithibitisha hilo kuna unyakuo wa Kanisa "utakuwaje?' Sifahamu, lakini atalithibitisha hilo, neno lake ni kweli (I Kor. 15:35-58). Kuna utawala wa miaka elfu, atalihakikisha hilo ni neno lake, kutakuwepo Ulimwengu mpya na Mbingu mpya (ufunuo 21:1) atalithibitisha hilo. Sababu neno lake limesema hivyo, wenye haki tu watakuwa pale atalithibitisha hilo, kwamba ni kweli. Wale tulio sehemu ya neno lake Unaona watakuwa na sehemu na nafasi katika neno kwa wakati wao. Watakuwa hao pekee pale sababu ndivyo ilivyo yeye ni neno, na Mwanamke ni nani? Sura ya mume, na Kanisa,ni mimi? sura ya neno (Mwa. 1:26-27, IKor. 15:49). Ona hilo kwa uhakika. Ona? kwa uhahika. Unaona? Ndivyo itaavyokuwa, ni sahihi. Waamini wa kweli tu wa neno watafahamu hilo na wataliamini na Mungu atawasaidia kuthibitisha hilo (Hiyo ni sawa). Hiyo ni kweli.

Sasa angalia, tarumbeta itawaita watu wajikusanye pamoja kwa ajili ya kitu fulani. Mara nyingine inatangaza mtu mashuhuri kama wa wakati wa Joseph. Wanapiga tarumbeta na Joseph anatokea. Ambayo ilikuwa ni ishara ya Baragumu kuu (tu ambayo tunazungumzia juu yake na tutaipata baada ya muda). Katika Isaya inasema kwamba wakati tarumbeta au Baragumu kuu italia Bendera itainuliwa juu nje kule. Hapo ndipo utakuja wakati Baragumu kuu italia na Mataifa yote watakusanyika Yerusalemu. Hapo ndipo utawala wa miaka elfu utaanza, Baragumu Kuu.

Na katika Isaya 27:12 na 13 ni hapo ambapo baragumu italia na Mataifa yote wataitambua Israeli kwenye nchi yao. Mungu pamoja nao. Hapo sasa Bibi arusi atakuja kuwa pamoja na Bwana arusi na Bwana arusi pamoja na Bibi Arusi (na baadaye utawala Mkuu wa miaka elfu , baada ya dunia yote kuharibiwa na nguvu za atomiki na kutakuwepo na mbingu mpya na nchi mpya) Tutaishi milele (Isaya 19:23 –25).

Shetani, mungu wa wakati huu kwa maarifa yake atawapa watu kula kutoka kwenye mti uliochanganyika wa mema na mabaya …………… angalia. Shetani kwa maarifa yake atasababisha watu wa kizazi hiki kiovu kula kwenye mti wa mema na mabaya, atasema anajenga ustaarabu mkubwa wa Ukristo kwa maarifa yake ya mema na mabaya, ustaarabu mkubwa wa Ukristo (Mwa. 3:1-5) lakini kundi dogo la Wakristo Bikira wa neno Bibi Arusi, hawatajali maarifa yake, hawataungana naye (Methali 3:5-6) Ni nini hiyo?

Sasa na tumzungumzie kwa muda? Anamngoja Bwana wake na sherehe ya Arusi ya miaka elfu (Hiyo ni kweli) pamoja na Neno Bwana Arusi kama ilivyo neno Bibi Arusi (Waebr. 9.27-28).

Kwasababu wakati Malaki 4, huo unabii utakapohubiriwa, dunia itateketezwa na moto mkali na wenye haki wote watatembea kwenye utawala wa miaka elfu, wakikanyaga majivu yao na hiyo haijatokea katika wakati wa Yohana.

Yuko wapi yule mmoja atakayepanda mbegu kwa Kanisa la wakati wa mwisho? Iko wapi mbegu iliyoiva,Eliya aliyeahidiwa na baada tu ya siku zake kutakuwa na mateso ya dhiki kuu yatakayoishia na kuchomwa moto kwa dunia.

Na pia baada ya kurudi kwa kanisa na Bibi Arusi Bibi Arusi na Kristo watakuwa wanatembea kwenye majivu ya waovu kwa miaka elfu, wakati dunia itakapotakaswa kwa moto. Na hapo watatawala. Wale Mataifa wote wasiosikia neno la Injili watafufuliwa wakati huo, na wana wa Mungu watadhihirishwa, kama atatawala lazima awe na kitu fulani cha kutawala. Watakuwa na Milki "Na wakatawala pamoja na Kristo na Kristo atatawala na fimbo ya chuma hapo Injili …… Wana wa Mungu waliodhihirishwa watakuwa na Mamlaka kama aliyokuwa nayo Bwana hapa. Hapo itakuja miaka elfu ya utawala juu ya majivu ya waovu (Rumi 8:18-21).

Tumekuwa na mapambano ya vita nyingi kubwa, Mapambano ya vita za kiroho, siku nyingi za ushindi (Vdays) ambalo Kanisa lilipata. Nina maanisha Kanisa, mwili wa Kristo, sizungumzi juu ya taratibu walizonazo madhehebu sasa. Ninazungumzia mwili wa Kristo, mwili wa waamini wakati wa nyakati zote wamekuwa na siku nyingi za ushindi.

Tumesikia vita mbalimbali, vita na Matetesi ya vita na siku za ushindi, na siku za ushindi na siku za ushindi na mwisho wake kumalizikia kwenye mapambano makubwa ya Armagedoni, hiyo ndio itakuwa mwisho wake. Wakati Atakapo kuja kwenye mapambano ya vita ya Armargedoni, hapo ndipo mwisho wa vita vyote.

Kabla tu ya utawalawa wa miaka elfu, Armagedoni ndiyo, itaisafisha dunia yote (Uf. 16:16) 19:11-16, Joel 3:1-2). Itajitakasa yenyewe kwa kujilipua na silaha za atomiki na majivu ya Volkano, na kitu hicho kitazamisha damu za watu zitanywea kwenye dunia, na dhambi, na maasi. Itazama ardhini au duniani, na Volkano itapasuka tena, na kuifanya dunia upya na kuisafisha tayari kwa utawala wa miaka elfu. Yeye anasafisha Kanisa la wakati huo kwa watu wake kuishi hapo. Ameni. Nasema, nalipenda hilo, ndio Bwana, utakuja wakati ambapo litakuwa kubwa.

Na wakati huo wa mwisho atakuwa Bwana Yesu mmoja na Bibi Arusi wengi. Mmoja, unalipata hilo? Kulikuwa na Daudi mmoja katika kiti cha enzi cha kifalme kimoja na Mfalme mmoja mwenye moyo kama wa Mungu na wanawake mia tano. Bwana Yesu ameketi katika kiti chake cha enzi cha ufalme wake (Haleluyah) kwenye utawala wa miaka elfu, pamoja na mke wake kama ilivyokuwa Mwanzo, alipoumba kutoka katika Dunia kwa mkono wa Mwenyezi Mungu kwenye ufufuo wa wafu, na watu wengi. Lione hilo pale.

Wakati wa utawala wa miaka elfu, Chui na Mwanambuzi watakula pamoja, Simba atakula mabua kama Ngombe na watalala pamoja na ndama (Isaya 11:1-10). Hawataumizana wala kuharibu kwenye utawala wa miaka elfu. Shetani ataondolewa (Ufu 20:1-3). Ni Shetani aliyewafanya wanyama wawe wakali wanauma, wanakamatana na kulana na mambo kama hayo jinsi wanafanya. Ni Shetani anayefanya hayo. Kama wote, (kwenye Kanisa la Laodikia) wao wangetambua ahadi ya ishara iliyowekwa ya Mesia. Ishara ya Mwana wa Adamu, atakuja kwa jina la mwana wa Adamu, sasa amekuwa katika jina kupitia nyakati za Pentekoste, katika Roho Mtakatifu, mwana wa Mungu sasa, kitu kifuatacho ni utawala wa miaka elfu, mwana wa Daudi, watoto watatu, Mungu yule yule Baba yule yule mwana na Roho Mtakatifu; Mungu yule yule, Mwana wa Daudi (Mat. 9:27,15:21-24, 20:30-31, (Luka 18:38-39) Mwana wa Mungu (Mt. Yon. 9:35-38, mat 14:33), Mat. 9:20) Mwana wa Adamu (Luka 18:8), 17:26-36, Mat 26:45) mwana wa Mungu ni Mungu yule yule wakati wote, kwenye Ofisi tatu za kazi.

Tunaona, baada ya kifo chake, mazishi na ufufuo alikuja kwenye siku za Pentekoste kama mwana wa Mungu yule Roho katika hali ya Roho Mtakatifu. Nini alichokuwa akifanya? Alikuwa akijibadilisha mwenyewe, amejifanya mwenyewe ajulikane kwa watu wake katika hali tofauti. Kama Roho Mtakatifu ambaye ni Mungu , alikuja kutenda kwenye nyakati za Kanisa kama mwana wa Mungu , Roho Mtakatifu lakini katika Utawala wa miaka elfu atakuja kama mwana wa Daudi kwenye kiti cha enzi cha Daudi Mfalme. Atachukua atachukua kiti cha enzi Daudi. Yupo kwenye kiti cha enzi cha Baba yake sasa, na Alisema, yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha
Enzi" kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi " (Ufu. 3:21) sasa yeye katika utawala wa miaka elfu atakuwa kama mwana wa Daudi itakuwaje? Mungu yule yule muda wote akijibadili sura yake.

Hilo ndilo tu tunalopaswa kujua Mungu ameahidi hilo, itakuwaje ? siwezi kulielezea lakini Mungu amesema hivyo atamtuma Yesu Kristo mara ya pili atakuja katika umbile linaloonekana atawachukuwa walio wake, kutakuwa na miaka elfu moja ya utawala wake duniani hapa pamoja na waliokombolewa. Hilo ndilo aliloahidi. Na tunangoja muda huo ufike. Mungu ndani ya Kristo akisikika amejifanya mwili, anakaa pamoja nasi. Na katika utawala ule mkuu wa miaka elfu ijayo, Mungu katika Umbo la Kristo amekaa katika Kiti cha enzi cha Daudi . (Isaya 9:6:7, 22:22, Luka 1:30-33) na Kanisa, Bibi Arusi wake, Bwana na Bibi pamoja.

Muda hautakoma mpaka ile …….. tunapata miaka elfu baada ya kanisa limekwenda nyumbani na kurudi tena duniani. Hapo sasa muda utakoma katika Mbingu mpya na nchi mpya (Efeso 1:10).

Sasa miaka elfu siyo mbingu mpya na nchi mpya kutakuwa na dhambi baada ya miaka elfu, Miaka elfu niulinganisho na wakati wa Nuhu kwenda kwenye Safina, imewabeba ikamleta hamu na wengine kwenye upande mwengine. Na dhambi ilitoka nje ya safina Unaona?

Lakini Enoki, mmoja aliye nyakuliwa, alikuwa ni mfano wa Bibi Arusi aliyekwenda juu, sio mmoja aliyeelea
(Heb 11:5-6). Hivyo dhambi bado itakuwepo katika upande mwingine wa utawala wa miaka elfu. (Ufu. 20:7-10) lakini sio katika utawala wa miaka elfu unaona? Wakati wa utawala wa miaka elfu ni amani. (Isaya 65:17-25).

Unaona? Lakini dhambi itashughulikiwa vilivyo kwa upande wa pili wa miaka elfu, na hapo muda utakoma. Katika utawala wa miaka elfu kuna Elohim amekaa kwenye kiti cha enzi na watu wake wote ambao wanamzunguka aliowafia kimbele kabla ya kuwekwa misingi ya Dunia .

Tumeliona, Kanisa, lililo vuguvugu, kitu chochote nje ya Bibi arusi aliyechaguliwa kitaenda kwenye kipindi cha mateso (dhiki kuu) hawatafufuliwa kwenye ufufuo wa kwanza, " Hao wafu waliosalia hawakuwa hai hata itimie miaka elfu" (Ufu 20:5). Wale tu waliochaguliwa kimbele walioteuliwa, Bibi Arusi mteule, uchaguzi wa Mungu mwenyewe.

Ni nani ndugu Branham? Sijui? Siwezi kukuambia ni nani lakini ninajua itakuwa hivyo. Sababu Mungu alisema itakuwa Unaona? Kuna watakao inuliwa juu kwenye kipindi cha mateso (Ufu. 3:10) lakini wote waliobaki wataingia kwenye kipindi cha mateso, wataenda chini, na kila kitu kitauwawa kabla ya mika elfu. Ndipo wenye haki watatawala katika utawala wa miaka elfu na wataishi miaka elfu.

Na baada ya miaka elfu, hukumu kuu ya kiti cheupe cha enzi itakuja na wote waliokufa, katika haki na katika makosa watafufuliwa, (Mat. 25:31-40). Na Vitabu vitafunguliwa na kitabu cha uzima kilifunguliwa, na watakatifu, Bwana na Bibi Arusi watakaa kuhukumu, Ulimwengu (Uf. 20:11-15). Na hapo utatimia usemi wa kusema atawahukumu Mataifa yote kwa fimbo ya Chuma" (Ufu. 2:26-28, Zab.2). Mataifa yote yatasimama mbele yake pale, na atayahukumu na fimbo ya chuma, atatenganisha kondoo na mbuzi na kuwaambia mbunzi ondokeni na kondoo njooni mliobarikiwa na Baba yangu.

Sasa hapo kutakuwa na kambi ya Mkutano wa Watakatifu katika mapana ya nchi, Na Shetani atafunguliwa kutoka kifungoni na atakwenda kupigana na watakatifu (Uf. 20:7-10) ndipo Mungu atanyesha moto na kibiriti kutoka Mbinguni , na Ulimwengu wote utamezwa kama ……. Utachomwa na kuharibiwa, hakutakuwa na bahari, hakutakuwa na maji hakuna kitakachobaki duniani. Volkano italipuka na kutawanyika na kuunguza vitu vyote………..

Kisha nikaona Mbingu mpya na nchi Mpya kwa maana Mbingu za kwanza, nchi dunia ya kwanza vimekwisha kupita hapana bahari tena nami Yohana nikaona mji ule Mtakatifu ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu umewekwa tayari kama Bibi Arusi kupambwa kwa mumewe , kumbuka hilo na katika huyo Bibi Arusi ….. "Tazama Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu na Mungu atakaa pamoja nasi kwenye umbile la mji sura ya piramidi yenye miraba wa maili elfu na mia tano na juu ya mji huo kutakuwa Mwanga au Nuru Amen. (Ufu. 21:27).

Swali Ndugu Branham ni wapi Bibi Arusi atakuwa wakati dunia itakapo lipuliwa na kuchomwa? Je itakuwa kama vile wana wa Israel walivyokuwa Gosheni wakati mapigo yakitokea?

Je Bibi Arusi atakuwa duniani wakati hayo yanatokea? Kama ndivyo, wapi, Je na Bibi arusi atakuwa mahali pamoja wakati wa kunyakuliwa.?

Wakati dunia itakapolipuliwa Bibi Arusi ……… muda wa unyakuo ndio muda wa kuamshwa kwa waliokufa na ni wakati wa kukusanyika pamoja walio hai, kwa maana walio hai kwa ……. unyakuo kufanyika. Sasa lakini Bibi Arusi…… sasa unaona, mmoja wao ni unyakuo nyuma hapa kabla ya utawala wa miaka elfu na baadae dunia itakapolipuliwa nyuma hapa baada ya utawala wa miaka elfu na baada ya hukumu ya kiti cheupe una ona? Watakatifu watakuwa kambini katika mapana ya dunia wakati Shetani atakapokuja kuuzanguka mji huo uliopendwa na Mungu atanyesha moto na kibiriti kutoka Mbinguni na kuwaharibu. Sahihi sasa hayo ni maandiko.

Kumbuka hapo sio muda mrefu ulipita, niliwafundisha juu ya Baragaumu saba, karamu ya Baragumu na nyinginezo? Na kama nilivyosema kuna siku nane za Karamu. Siku ya saba itakuwa ni ya mwisho. Hiyo ndiyo itakuwa utawala wa miaka elfu. Lakini kutakua na karamu ya (8) nane. Ambayo kama ni siku ya nane, na kunakuwa na siku saba tu , itakuwa inafanya siku ya kwanza tena inarudi kwenye siku ya kwanza. Hapo baada ya miaka elfu kwisha, hapo ndio kuanzishwa tena kwa bustani ya Edeni Ufalme wa Mungu utakuwa umerudi tena sababu Yesu alipigana na shetani bustani ya Gethemane na kushinda kuirudisha Eden tena. Ambayo amekwenda kuiandaa Mbinguni ili kurudisha tena. Juu Mbinguni alisema " Msifadhaike mionyoni mwenu (Yoh. 14:1-3, 16:33).

Swali, wakati wa mwisho wa kanisa unaishia umetiwa giza bibi arusi ameitwa, Je tumeingia kwenye kipindi cha mateso?

Hapana hapana una ………. Natamani sana kwamba ningekuwa na muda katika hilo, Unaona Unaona? Bibi Arusi, atakapochukuliwa kutoka Kanisani, kipindi cha Kanisa kitakoma. Laodikia itaingia kwenye machafuko . Bibi Arusi anakwenda kwenye utukufu, kipindi cha dhiki kuu itakuja kuwa kwa mwanamwali mpumbavu kwa kipindi cha miaka mitatu na nusu wakati huo Israeli wanapata unabii wao na dhiki kuu itaingia kwa Israel, na kutakuja kipindi cha vita ya Armagedoni, ambacho kitaharibu kila kitu. Na Bibi Arusi atarudi na Bwana Arusi kwa miaka elfu, utawala wa miaka elfu. Baaada ya hapo tutakuja kwenye hukumu ya kiti cheupe, Baada ya hapo itakuja Mbingu mpya na nchi mpya, Mji ule mpya utashuka chini kutoka kwa Mungu toka Mbinguni. Wakati na umilele vitachanganywa pamoja.

Nukuu.za kiingereza :
“ Kutoka kwa tatu” uk. 17,43-45/ Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 83.
“ Nitawezaje kushinda” Ay. 61”Mhuri wa Saba” Aya 386 – 391.
Maswali na majibu (64-083e), utaratibu na mwenendo wa Kanisa uk. 1165,1167, 1173,1160, swali namba 404, 406, 415,392 nenda kamuonyeshe Yesu (63-1103) Aya E-48/kuthibitisha neno lake 64-0816, Aya 232 karamu ya baragumu uk. 21 + 42/ Mungu wa kizazi hiki kiovu Aya 126.

Kitendawili (64-0206b) Aya 111/maswali na majibu (62-0527), utaratibu na mwenendo mafundisho uk 723 Aya 177 –178, siku ya ushindi aya E-50/ Ndoa na talaka, Aya 38, yeye aliye ndani yenu 963-1110e). Aya 176/, kutambua siku yako na ujumbe wake, Aya 123; mzee Ibrahimu Aya 14 Bwana, tunataka kumwona Yesu (64 – 0304), para 18, maswali na majibu (64-0830m) utaratibu namwenendo mafundisho Uk 1092 Aya 142, Mungu Mkuu afunuliwa 64-0629 page 9) kufunuliwa kwa Mungu (64 – 0614M) Aya 83 – 84, Edeni ya Shetani Aya 165/maswali na majibu (64-083E); utaratibu na mwenendo mafundisho 1045, 1010 Aya 233-236, 284

---

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 130 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii yamekusanywa na Gerd Rodewald frienderstr. 69D -75328 Sehomberge Germany simu (+49) 72357613 Fax 72353306

---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na Mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Nd. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*